# Ofisi Ya Rais - Tamisemi

# Halmashauri Ya Manispaa Ya Tabora

# Jarida La Halmashauri

Toleo Na. 1. | Septemba 2020

## MAFANIKIO YA MIAKA MITANO YA SERIKALI YA AWAMU YA TANO HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA



Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli

**Rais Wa Jamhuri Ya Muungano Wa Tanzania**



Mhe.Samia Suluhu Hassan

**Makamu Wa Rais**

**Jamuhuri Ya Muungano Wa Tanzania**



Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa

**Waziri Mkuu**

**Jamhuri Ya Muungano Wa Tanzania**

## BODI YA UHARIRI

**Bosco O. Ndunguru**
Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora

**Emmanuel S. Dyelu**
Kaimu Mchumi Manispaa ya Tabora

**Paul P Kasembo**
Afisa Habari Manispaa ya Tabora

## MAWASILIANO

S. L. B 174 Tabora

Simu +255786820518

Nukushi +255262604835

Baruapepe: md@taboramc.go.tz

## MITANDAO YA KIJAMII

www.taboramc.go.tz



## NENO KUTOKA KWA MKURUGENZI MKURUGENZI

Bosco O. Ndunguru

### MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA.

Natoa shukurani zangu za dhati na pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa imani yake kwangu na hata akanipa dhamana ya kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

Pia natoa shukurani zangu za dhati kwa Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mhe. Selemeni Jafo (Mb), Mkuu wa Mkoa wa Tabora Mhe. Aggrey Mwanri, Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora Ndg Msalika Makungu, Mkuu wa Wilaya ya Tabora Mjini Mhe. Komanya Kitwala kwa uongozi wao mzuri, ushirikiano wanaonipatia wakati wote kwenye kutekeleza majukumu yangu ya kazi nawashukuru sana. Bila kumsahau Mstahiki Meya wa Mnaispaa ya Tabora Mhe. Leopold Ulaya, Mbunge wa Tabora Mjini Mhe. Emmanuel Mwakasaka, Mhe Munde Tambwe Mbunge V/M, Mhe. Mwanne Mchemba Mbunge V/M, Mhe. Hawa Mwaifunga Mbunge V/M, Mhe. Rehema Migila Mbunge V/M, Katibu Tawala wa Wilaya ya Tabora Mjini Ndg Hammarskjold Yonaza pamoja na Waheshimiwa Madiwani wote wa Baraza la Madiwani Tabora Manispaa kwa ushirikiano wao mkubwa wananonipatia wakati wote.

Halmashauri ya Manispaa ya Tabora inaendelea kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi watumishi wake kwa ujumla na kwa kuzingatia Misingi ya Utawala Bora pia Uwajibikaji.

Kwa kuzingatia hayo yote Halmashauri imeweza kutatua kero nyingi kutoka kwa wananchi na kwamba inaendelea kuzipatia ufumbuzi katika ngazi mbalimbali kuanzia Halmashauri, Kata, Mitaa, Vijij na Vitongoji ikiwa na kusudio la kuhakikisha wananchi wote wanakuwa hawana kero ili waweze kufanya kazi na shughuri zao ambazo zinawapatia kipato chao na hatimae waweze kuinuka kiuchumi pia waweze kuenenda na malengo ya Nchi na kuifikisha Tanzania kwenye Uchumi wa kati kama ilivyo dhamira ya Mhe Rais John Pombe Magufuli.

Kwa upande mwingine Halmashauri ya Manispaa ya Tabora imejiwekea mkakati wa kuongeza vyanzo vya mapato jambo ambalo litachagiza na kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa kumfikia kila anayestahili kulipa kodi. Sambamba na hilo pia mapato yameongezeka zaidi baada ya kuanza kwa matumizi ya ukusanyaji kwa kutumia mashine maalumu za kielekitroniki badala ya kukusanya kwa kutumia vitabu kama ilivyokuwa awali.

**Hitimisho**, mipango iliyopo kwenye Halmashauri yetu kwa sasa ni pamoja na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya unaoendelea hivi sasa, matarajio ya ujenzi wa Stendi mpya ambayo itakuwa ya kisasa zaidi, ukarabati wa Soko kuu kuwa la kisasa zaidi pamoja na ujenzi wa Machinjio ili iwe bora na ya kisasa zaidi tofauti na ilivyo sasa hivi. Aidha Halmashauri imeweza kujenga Maduka mapya 24 yaliyopo stendi ya mabasi, ujenzi wa Soko la kuteremshia mazao ya nafaka na matunda-Tambureli, soko jipya la mbao litakalokuwepo eneo la Transfoma kata ya Ipuli. Hivi ni baadhi tuu ya vyanzo vikubwa vya mapato ambavyo vitaenda sambamba na uboreshwaji wa huduma kwa wananchi na kwamba kwa kufanya hivyo kutaipandisha hadhi Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kwa siku zijazo. ASANTENI SANA.

*JIPATIE NAKALA YA CHAPISHO HILI KWA KUPAKUA KUTOKA KWENYE TOVUTI YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA* ***www.taboramc.go.tz***

# IDARA YA UCHUMI, TAKWIMU NA UFUATILIAJI

Idara hii ni moja kati ya Idara zinazounda Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ambayo ina jukumu kubwa la kuandaa na kutekeleza Mipango ya Halmashauri ili iweze kusonga mbele kulingana na mikakati iliyojiwekea na sera za Wizara na Nchi kwa ujumla.

Idara hii kwa kipindi cha Miaka mine ya Serikali ya Awamu ya Tano imeweza kufanya yafuatayo; Halmashauri ya Manispaa imefanikiwa kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuboresha vyanzo vilivyopo vyenye dhamira ya kuziba akisi iliyopo. Kwa sasa tayari Halmashauri imeainisha Miradi ya kiuwekezaji pamoja na maeneo ambayo uwekezaji huo unaweza kufanyika kupitia kijitabu cha Muongozo wa Uwekezaji cha Mkoa wa Tabora **(Tabora Investment Guide).** Uzinduzi wa kitabu hicho utafanyika mwezi Februari 2020.



**Soko Jipya La Mbao Lililopo Transifoma – Ipuli**

Hadi sasa tayari Mpango wa Uwekezaji Kimtaji yaani **Capital Investment Plan (CIP)** umekwisha andaliwa ambao unajumuisha Miradi ya vipaumbele 38 kutoka katika Sekta mbalimbali za utoaji huduma, kujenga uwezo, Viwanda, Masoko, Maegesho ya magari makubwa, Elimu na Afya, Michezo nk, na maandiko 14 yamekwisha aandaliwa kwa ajili kutafuta wawekezaji.

Katika kuiandaa na kuiweka Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ili iweze kuakisi kasi na malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano, pameundwa Kamati ya Uwekezaji inayojumuishaa wataalamu wafuatao; Mchumi wa Manispaa ni Mwenyekiti, Afisa Mipango Miji ni Katibu, na Wajumbe ni Mwanassheria wa Manispaa, Afisa Manunuzi, Mhandisi wa Ujenzi, Afisa Maendeleo ya Jamii na Mweka Hazina. Kamati hii itakayokuwa na jukumu kubwa la kuhakikisha masuala yote ya Uwekezaji yanafanikiwa na kutekeleza kwa kiwango cha juu kama inavyotarajia Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.



**Muonekano Wa Upande Wa Ndani Wa Soko La Mbao**

"Sisi kama Idara kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Tabora imejipanga kuendelea kutoa huduma za kiushauri za kitaalamu zenye mlengo wa kuiwezesha Halmashauri kufikia malengo ya jamii inayoihudumia, kuinua uchumi wa Halamashauri na Serikali kwa wananchi wake pia kuendana na mikakati ya kimazingira nk mambo ambayo yataendana na lengo la Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. John Pombe Magufuli ya kuifanya Tanzania kuwa yenye Uchumi wa Kati'', alisema Emmanuel Dyelu.

Sambamba na mikakati hiyo, Halmashauri pia imekwishaandaa maandiko Miaradi matatu (3) kwa jaili ya kutafuta fedha kutoka kwa wafadhili yakiwa tayari kwa ajili ya kuwasilisha OR-TAMISEMI na Wizara ya Fedha kwa ajili ya maombi ya fedha, Miradi hiyo ni; (i) Ujenzi wa Soko Kuu la Manispaa, (ii) Ujenzi wa Stendi Kuu ya mabasi ya kisasa na (iii) Ukarabati wa Machinjio ya Kisasa ikiwa na mashine ya kuchinjia ndani yake.

# UTEKELEZAJI WA MRADI WA UBORESHAJI MIJI NA MANISPAA (ULGSP) CHINI YA UFADHILI WA FEDHA ZA BENKI YA DUNIA HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA.

## 1.0 UTANGULIZI

Halmasuari ya Manispaa ya Tabora ni moja kati ya Halmashauri 18 Tanzania bara inayotekeleza mradi wa uboreshaji miji na Manispaa ambapo ulianza utekelezaji wake mwaka 2013/2014. Mradi ulilenga kuzijengea uwezo Halmashauri ili ziweze kujitegemea katika masuala ya usimamizi wa rasilimali fedha, utawala bora, uimarishaji wa miundombbinu na usimamizi mzuri wa mikataba na miradi ya maendeleo.

## 2.0 TAARIFA ZA FEDHA

Tangu kuanza kwa mradi hadi mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Manispaa ya Tabora imepokea na kutumia jumla ya shilingi 30,152,175,410.977 kwa ajili ya shughuli zifuatazo; ujenzi wa barabara kiwango cha lami nene (Asphalt concrete) zenye urefu wa km 21.35, uandaaji wa mpango kabambe wa Tabora Manispaa (Master plan 2012-2032), ununuzi wa mitambo mbalimbali kwa ajili ya usafi wa mji, kuwalipa wakanadasi washauri (Consultacy services) za; Ujenzi wa stendi mpya ya mabasi, uthamini wa majengo kwa ajili ya tozo ya kodi ya majengo na kutoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa waheshimiwa Madiwani na wataalamu wa Halmashauri

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MRADI WA UJENZI WA BARABARA ZENYE UREFU WA KM 21.35

Ujenzi wa barabara kiwango cha lami nene umejegwa kwa awamu tatu tofauti (three phases) kama ifuatavyo;

### 3.1 Ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 6.1

Halmashauri imefanikiwa kujenga barabara zenye urefu wa km 6.1 awamu ya kwanza (LOT 1) chini ya mkandarasi M/S SALUM MOTORS TRANSPORT Co. LTD and ANAM ROAD WORKS Co Ltd na Mkandarasi Mshauri Advance Engineering Solutions katika barabara za; Rehani (km 1.525), Manyema (km 1.3), Migazi (km 0.95), Kanyenyera (km 1.405), Usagara (km 0.4) na Kazembe (km 0.52). Ujenzi wa barabara hizo umekamilika asilimia 100 kwa gharama ya **shilingi 8,222,664,626.00**

### 3.2 Ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 9.23 (LOT 2)

Halmashauri imefanikiwa kujenga barabara zenye urefu wa km 9.23 awamu ya pili (LOT 2) chini ya mkandarasi M/S SALUM MOTORS TRANSPORT Co. LTD and ANAM ROAD WORKS Co Ltd na Mkandarasi Mshauri Advance Engineering Solutions katika barabara za; Mapambano (km 2.06), Magereza (0.960, Hill (km1.28), Kazehill (km 2.33), Gongoni (km 0.520, Salmin (km 0.51), Tautugawe (km 0.29), Sabasaba (km 0.650 na Magereza (km 0.63) Ujenzi wa barabara hizo umekamilika asilimia 100 kwa gharama ya **shilingi 11,589,220,841.25**

### 3.3. Ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 6.02 (LOT 3)

Halmashauri imefanikiwa kujenga barabara zenye urefu wa km 6.02 awamu ya tatu (LOT 3) chini ya mkandarasi CHONGQING International Construction Corporation (CICO) na Mkandarasi Mshauri Advance Engineering Solutions katika barabara za; Kuya (km 1.78), Majengo (km 2.89), Nyerere (km 0.59), Transformer (km 0.49) na Heri (km 0.27). Ujenzi wa barabara hizo umekamilika asilimia 100 kwa gharama ya **shilingi 6,720,785,053.20.** Kuwepo kwa mradi huu katika Halmashauri yetu ya Manispaa ya Tabora kumeongeza tija katika uzalishaji, usafirishaji wa bidhaa kutoka eneo moja hadi lingine., pia umesaidia kuboresha muonekano wa mji wa Tabora.

# EQUIPMENTS





***Lori mbili zikiwa kwenye Utekelezaji***





***Gari maalumu kwa ajili ya kubebea kontena za taka ngumu***





***Mtambo maalumu kwa ajili ya kuchimba na kupakia***





***mitambo maalumu kwa ajili ya kutengeneza bara baraMotor Grader***

# IDARA YA ELIMU SEKONDARI

Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ina jumla ya shule za sekondari za Serikali ambazo katika kipindi cha miaka mine ya Serikali ya Awamu ya Tano zimekuwa na msaada mkubwa sana hasa kwenye kuhakikisha wananfunzi wote wanaomaliza darasa la saba wanaendelea na elimu ya sekondari ili kuachana na dhana ambayo ilikuwa imejengeka hapo awali ya kwamba mwanafunzi akaimaliza darasa la saba aweza kubakia nyumbani kufanya kazi za shamba, kuchunga mifugo au kuolewa kwa upande wa wasichana.

Ndani ya kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya awamu ya tano Tabora Manispaa imeweza kupata kiasi cha **Tzs994,863,758.13/=** kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe nne (4) ambazo ni Tabora Wavulana Tabora Wasichana **Tzs 998,563,003/=** Milambo **Tzs 522,072,250/=** na Kazima **Tzs 899,206,435/=**.




**Muonekano mpya wa shule kongwe ya Tabora wavulana (Tabora boys)**

Pia Serikali ya awamu ya tano ndani ya miaka minne imeipatia Manispaa ya Tabora kiasi cha **Tzs 25,500,000/=**kwa shule ya sekondari ya Chang'a iliyopo Kata ya Tumbi kwa ajili ya kukamilisha vyumba viwili vya madarasa na **Tzs 25,500,000/=** kwa shule ya sekondari ya Bombamzinga iliyopo Kata ya Mtendeni ikiwa ni kwa ajili ya kukamilisha vyumba vitatu vya madarasa.

Kutengenezwa kwa madawati **2062** kwa ajili ya matumizi ya shule zote **23** za serikali zilizopo Tabora Manispaa pamoja na kutengeneza vitanda **100** kwa matumizi ya shule ya Tabora Wasichana ikiwa na dhamira ya kuondoa adha waliyokuwa wakiipata wanafunzi.



**Baadhi ya madarasa Shule ya Tabora Wasichana (Tabora Gilrs)**

Sambamba na yote hayo, Serikali ya awamu ya tano ndani ya kipindi cha miaka mitano imeweza kuanzisha ujenzi wa mabweni kwa ajili ya wanafunzi wa kike katika shule ya Itonjanda iliyopo kata ya Itonjanda, Ndevelwa iliyopo kata ya Ndevelwa, na Itetemia iliyopo kata ya Itetemia ikiwa na lengo la kuboresha mazingira yawe rafiki zaidi kwa wanafunzi jambo ambalo halikuwa kufanyika hapo awali.

Mafanikio hayo yanachagisha kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaosajiliwa, ambapo kwa mwaka 2015 kulikuwa na wanafunzi **10,329** hadi kufikia **17,401** kwa mwaka **2019** ikiwa ni ongezeko la asili



mia **68.** Aidha kumekuwa na ongezeko kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na kidato cha Tano ambapo mwaka **2015** kulikuwa na wanafunzi **774** mpaka kufikia **1,053** kwa mwaka **2019** ikiwa ni ongezeko la asilimia **36.**

"Kwa kweli naishukuru sana na kuipongeza Serikali ya awamu ya tano kwa namna ambavyo imefanya mabadiliko na kuleta matokeo makubwa yanayoakisi uhalisia na kukidhi matarajio ya wananchi wa Manispaa ya Tabora kwa upande wa Elimu ya Sekondari ndani ya kipindi cha miaka mitano na kuifanya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kuwa bora zaidi tofauti na awali,'' alisema Chatta Luleka ambae ni Afisa Elimu Sekondari.

Aidha katika hatua nyingine Afisa Elimu aliishukuru sana Serikali ya awamu ya Tano ambapo kwa kipindi cha miaka mitano iliweza kulitazama suala la upungufu wa waalimu hasa wa masomo ya Sayansi ambapo walileta walimu wapatao …. Ili kuinua









**Picha zikionyesha baadhi ya mjengo ya shule ya wavulana Milambo ikiwa ni muendelezo wa ukarabati wa ukarabati wa shule kongwe Tabora manispaa.**

## *FEDHA ZA EP4R 2019/2020*

**SHULE YA SEKONDARI MILAMBO TZS 732,072,250/=**

Awamu ya kwanza ni ukarabati wa mabweni 3, ukarabati wa madarasa, vyoo, jingo la Utawala, maabara, maktaba, bwalo la chakula ambapo jumla ya Tzs 522,072,250/= pamoja na ujenzi wa vyumba 04 vya madarasa. Kukamilika kwa kazi hiyo kutawezesha kuwa na mazingira bora ya kufundishia, kulala/mabweni, kufanyia kazi kwa waalimu, kuondoa msongamano kwenye vyumba vya madarasa.

**SHULE YA SEKONDARI KAZIMA 899,206,405/=.**

Shule ilibahatika kupata kiasi tajwa hapo juu kwa ajili ya ukarabati wa miundombinuyote ya Shule na Ujenzi wa Uzio kuzunguuka eneo la shule. Na kwamba upatikanaji wa fedha hizi kwa kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano kunapelekea shule ya Kazima kuwa na mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia pamoja na kuimalisha ulinzi wa wanafunzi wenyewe, mali zao na rasilimali zote kwenye shule ya Kazima.

**SHULE YA WASICHANA TABORA 998,563,003/=**

Katika ipindi cha serikali ya awamu ya Tano shule ya sekondari Kazima ilibahatika kupata kiasi cha Tzs 998,563,003/= kwa ajili ya ukarabati wa mabweni 25, mfumo wa maji taka na safi, vyoo 08, maabara ya kemia, biolojia. Ambapo kutawezesha kuwa na mazingira bora ya kufundishia, kujifunzia na kufundishiwa. Kuwa na mazingira bora ya kuishi/mabweni na kuondoa upungufu wa miundombino ya shule.

**SHULE YA SEKONDARI KANYENYE TZS 9,000,000/=**

Shule ya Sekondari Kanyenye imeweza kupata kiasi cha Tzs 9000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa matundu 05 ya vyoo vya wasichana jambo ambalo litapelekea kuboresha mundombinu na kuondoa upungufu kwa shule.

**SHULE YA SENDARI TABORA WAVULANA TZS 994,843,758,13/=**

Kwa kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya JPM, Shle ya Sekondari Tabora Wavulana ilipata faida kubwa kwa kupewa pesa kiasi cha Tzs 994, 843,758,13/= kwa ajili ya ujenzi wa maktaba, ukarabati wa maktaba ya zamani, ofisi 11, matundu 16 ya vyoo, madarasa 18, miundombinu ya umeme, maji taka na safi. Serikali ya awamu ya tano nchini ya Mhe JPM hakika Tabora Boys imekuwa na uhakika wa kuwa na mazingira bora ya kufundishiwa wanafunzi, kufundishia waalimu lakini pia uhakika na usalama.

**SHULE YA SEKONDARI BOMBAMZINGA TZS 25,000,000/=**

Serikali ya awamu ya tano imesaidia na kuiwezesha shule ya sekondari Bombamzinga kiasi cha Tzs 25,000,000/= kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba 03 vya madarasa na samani zake.

**SHULE YA SEKONDARI CHANGÁ TZS 25,000,000/=**

Ukamilishaji wa vyumba 02 vya madarasa na samani zake jambo ambalo limewezesha kuwa na mazingira bora, rafiki na yenye mvuto kwa kujifunzia wanafunzi.

**SERIKALI YA AWAMU YA TANO CHINI YA MRADI WA SEDP.**

1) SHULE YA SEKONDARI CHEYO MRADI WA SEDP TZS 132,000,000/= Katika kipindi cha miaka mitano ya serikali ya JPM, halmashauri ya Manispaa ya Tabora kupitia shuke ya Sekondari Cheyo imeweza kupata fedha Tzs 132, 000,000/= kwa ajili y ujenzi wa vyumba 04 vya madarasa na matundu 08 ya vyoo.

2) SHULE YA SEKONDARI ISEVYA TZS 82,000,000/= Kupitia mradi huo shule ya sekondari Isevya iliweza kujenga vyumba vya madarasa 02 na matundu ya vyoo 8.

3) SHULE YA SEKONDARI IPULI TZS 82,000,000/= Sekondari ya Ipuli I moja kati ya shule zilizonufaika na Serikali ya awamu ya tano, ambapo waiweza kupatiwa kiasi tajwa hapo juu kwa lengo la kujenga vyumba 02 vya madarasa na matundu 08 ya vyoo. “Naishukuru sana serikali ya awamu ya tano chini Mhe JPM kwani haya yote ni matokeo ya utawala bora na unaoijali sana sekta ya elimu, jambo ambalo limeifanya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kupaa kielimu, kuimarisha na kuanzisha mazingira bora ya kusomea wanafunzi sambamba na mazingira bora ya kufundishia hasa kwa upande wa waalimu”, Mwl Chatta Luleka, Afisa Elimu Sekondari Tabora Manispaa.

# IDARA YA AFYA



**Jengo la wodi – kituo cha afya Mailitano**

Kwa kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya awamu ya tano imefanya juhudi na kazi kubwa sana kwenye uboreshaji mkubwa kwenye sekta ya afya ambapo Serikali kuu ilitoa kiasi cha zaidi ya milioni mia nne kwa ajili kupanua kituo cha afya kimoja Mailitano kilichopo Kata ya Ipuli. Ambapo pia Halmashauri kupitia mapato yake ya ndani walitoa zaidi ya milioni themanini na kwa upande wa idara ya afya walitoa zaidi ya milioni ikiwa ni muendelezo wa upanuzi wa kituo hicho cha afya, ikiwa ni pamoja na kuongeza majengo mengine kutoka yale yaliyokuwepo awali na kukamilisha ujenzi huo wa kituo cha afya ambapo ndani yake kuna majengo ya maabara, jengo la kuhifadhia maiti, wodi ya akina mama,watoto, wazazi na wodi ya wanaume. Kukamilika kwa kituo hicho cha afya kutawezesha kuhudumia wagonjwa wengi na hivyo kuondoa msongamano kwenye hospitali ya Rufaa Kitete.



**Nyumba Ya Mganga Wa Kituo Cha Afya Mailitano**

‘’ Pamoja na mambo hayo mazuri ambayo yameboresha huduma za afya kwa wananchi wa Manispaa ya Tabora kutoka kwa Serikali ya awamu ya tano, lakini Halmashauri ya Manispaa kupitia mapato yake ya ndani imeweza kutoa vitambulisho zaidi ya 11,420 kwa ajili ya wazee wenye zaidi ya umri wa miaka sitini na wale wasiojiweza vyenye lengo la kuwawezesha kupata huduma ya matibabu bure ikiwa ni pamoja na kutenga dirisha maalumu na mahususi kwa ajili ya kuwahudumia wazee jambo ambalo litapunguza msongamano mkubwa wa wagonjwa kwenye Hospitali na vituo vingine vya afya vilivyopo hapa Manispaa,’’ alisema Mkurugenzi Bosco Ndunguru.

Aidha Ndunguru aliendelea kuelezea ya kwamba, kutokana na umuhimu wa sekta yenyewe ya afya ambayo inagusa maisha ya wananchi moja kwa moja hivyo Halmashauri ya Manispaa inaendelea na uboreshaji wa huduma za afya kwenye Zahanati zilizopo. Pamoja na maboresho hayo ya huduma, lakini pia Halmashauri kupitia mapato yake ya ndani kwa kushirikiana na Serikali ya Wilaya, wananchi, pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo inatarajia kuanza ujenzi wa Zahanati tatu kwenye kata za pembezoni ikiwemo Kabila, Ndevelwa. Sambamba na hilo, Serikali ya awamu ya tano imetupatia wataalamu mbalimbali wa afya wakiwemo wa madaktari, manensi (wauguzi) na wahudumu.

Aidha Elimu ya Afya ya jinsi ya kujikinga na VVU, kufanya upimaji na huduma za mafunzo kwa waathirika inaendelea kutolewa kwa kushirikiana na wadau wa EGPAF, JHPIEGO/SAUTI kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za Afya kwenye mikutano ya hadhara, kwenye maeneo ya kutolea huduma za kijamii kama vile Masoko, Shule n.k. Maambukizi ya VVU katika Wilaya ya Tabora ni 4.3% ukilinganisha na 3.6% ya Kitaifa. Sambamba na hayo, lakini pia ujenzi wa Kituo cha Afya Mailitano kilichopo Kata ya Ipuli kimekamilika kwa asilimia 100% ya ujenzi ikiwa ni utekelezaji wa malengo ya Srekiali ya Awamu ya Tano ya kuhakikisha kuwa lengo la kuboresha, kuimarisha na kusogeza huduma za afya kwa wananchi zinapatikana wakati wote.

Hata hivyo ndani ya kipindi hiki cha miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano, ndipo kiwango cha mapato ya idara ya afya yameongezeka hasa baada ya kuanza kutumika kwa mfumo wa malipo ya kieletroniki sambamba na kuhamasika kwa wananchi kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF na chf ILIYOBORESHWA) ambapo sasa umepunguza kwa asilimia kubwa sana malipo yaliyokuwa yakifanywa kwa pesa taslim.



**Sehemu ya Muonekano wa Ndani Kituo Cha Afya Mailitano**



**Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Tabora Mjini iliyopo Mtaa wa Uledi Kata ya Mpela**

# IDARA YA ELIMU MSINGI



**Jengo la shule ya msingi Bomba mzinga iliyopo Kata ya Isevya Manispaa ya Tabora**

Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ina jumla ya shule za msingi 73 ambapo kila shule ina darasa la awali, ambapo pia elimu bila malipo imetekelezekwa na mfumo unaotumika ni (2-7-4).

Kwa upande huu wa Idara ya Elimu Msingi ndani ya kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano Idara imeendeleakujivunia mafanikio makubwa yaliyofanywa na Serikali  hususani kwenye kwenyekuhakikishakuwa kuna msingi wa mwanafunzi unajengwa vizuri kwa kuboresha mazingira na kuimarisha namna ya kujifunzia sambamba na kufundishia baada ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kupatiwa fedha za kutosha kutoka kwa wafadhirli wa EP4R na EquipT ambapo walijikita katika ujenzi wa madarasa katika maeneo mengi hapa Manispaa ya Tabora ambapo kukiwa na lengo kuu la kupunguza umbali mrefu kwa wanafunzi waliokuwa wakitokea majumbani kwao hususani kwa madarasa ya awali mpaka darasa la pili.

Furaha yetu kwa kipindi cha miaka mitano ya utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuwa tumeweza kupokea kiasi cha fedha za Kitanzania shilingi **846,571,050.00**kupitia mradi wa EquipT na EP4R zenye lengo la kujenga vyumba sita vya madarasa na ofisi 3 katika shule za Msingi Igosha na Kapunze vilivyogharimu kiasi cha shilingi **133,200,000.00**. Ujenzi wa shule shikizi katika kata ya Itonjanda, Misha, Uyui na Tumbi zilizogharimu kiasi cha shilingi  **240,000,000.00,** na  kiasi cha shilingi **473,371,050.00** Kwa ajili ya umaliziaji wa maboma katika shule  za Majengo, Kizigo, Kapunze, Igosha, Ntalikwa, Ikomwa, Kipera, Miyemba,Umanda, Milambo barracks, Bombamzinga, Mpepo, kanyenye, Cheyo A, Kalunde, Magoweko, Uyui, Kwihara,Usule, Isike na Itema. Pamoja na yote hayo, pia kumefanyika ujenzi wa Ofisi za waalimu ambapo majengo yote yamekamilika,” alisema Mkurugenzi Ndunguru.





**Shule Ya Msingi Miyemba Iliyopo Kata Ya Mbugani**



**Picha Ikionyesha Madawati Ya Shule Shikizi Imalamihayo – Kata Ya Uyui**



**Shule Shikizi Imala Mihayo – Kata Ya Uyui**



**Shule Ya Msingi Uyui Iliyo Kata Ya Uyui Manispaa Ya Tabora**



**Shule Ya Msingi Magoweko Iliyopo Kata Ya Kakola**

# IDARA YA MAENDELEO YA JAMII

Serikali ilitoa maelekezo ambayo yalipitishwa kisheria kuhakikisha ya kwamba kila Halmashauri inatenga asilimia kumi (10) ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo kwa Wanawake asilimia 4, Walemavu asilimia 2 na Vijana asilimia 4, Serikali ilikuwa na lengo la kuhakikisha kuwa makundi yote yanakuwa na shughuli ambayo inawaingizia kipato jambo ambalo litapelekea kuomgeza kipato kwa lengo la kujikomboa kiuchumi ili hatimae waweze kuachana na utegemezi.

“Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kwa upande wake haikuchelewa hata kidogo kwenye kutekeleza agizo hilo la Serikali na kwa kipindi chote hiki cha miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano mpaka kufikia September 2020. Manispaa ya Tabora ilikuwa imetoa kiasi cha shilingi milioni mia tano tisini na tisa na laki sita (599,600) ambayo ni kuanzia mwaka 2016 kwa vikundi 369 vinavyojishughulisha na kazi za Ufugaji wa kuku, utengenezaji wa samani, kilimo cha umwagiliaji, ushonaji nguo, uselemala na utunzaji wa mazingira pamoja na mazao ya usindikaji”, alieleza Mkurugenzi Ndunguru.



**Picha Inaonyesha Kikundi Cha Jukwaa La Vijana Kata Ya Chemchem Tabora Manispaa.**

# IDARA YA UTAWALA NA UTUMISHI

Idara ya Utawala na Utumishi ni moja ya Idara zinazounda Halmashauri ya Manispaa ya Tabora yenye mamlaka ya kushughulikia masuala yawatumishi na kuhakikisha mambo ya Utawala bora yanatimizwa kwa watumishi ikiwemo kushughulikia stahili za watumishi.

Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi Bi. Christina Bunini anaelezea mafanikio yaliyopatikana katika Idara hiyo kwa kipindi chamiaka mitano.



**Baadhi Ya Wenyeviti Wa Mitaa, Vijiji Na Vitongoji wakiwa kwenye kikao kazi kilichoongozwa na Mkuu wa Wilaya Tabora Mjini, Mhe Komanya E. Kitwala (Hayupo Pichani)**

"Kwa kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano, Idara imeendelea kupokea watumishi kutoka Sekretarieti ya Ajira ambapo kama Idara tuliwapokea kwa niaba ya Mkurugenzi na kufanyiwa taratibu zote kama waajiriwa wapya ili kuhakikisha wanapata mishahara kwa wakati. Pia kwa kipindi hicho Idara ilipokea watumishi kwa ajili ya Idara mbalimbali zikiwemo Idara ya Afya watumishi 19, Elimu Msingi watumishi 21, na Idara ya Utawala watumishi 46," alielezea Afisa Utumishi Christina. Aidha Bi Christina aliendelea kutoa ufafanuzi kuwa Idara imehakikisha masuala ya kiutawala yanafanyika ili kutekeleza dhana nzima ya Utawala Bora katika ngazi zote katika Manispaa ya Tabora ukianzia ngazi ya Kata, Mitaa na Vijiji kwa kufanya usimamizi wa vikao vya kisheria katika ngazi hizo, kusimamia ulinzi na usalama katika maeneo hayo ikiwa ni pamoja na kuandaa vikaovyote vya kisheria ngazi ya Halmashauri.

"Pia Idara hii ya Utawala inasimamia dawati la malalamiko ambalo lipo chini ya mtumishi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii ambapo hupokea malalamiko ya wananchi na kuyatafutia ufumbuzi ambapo kwa sehemu kubwa yalihusu Idara ya Ardhi, hivyo yaliwasilishwa Idara husika na yalifanyiwa kazi na yale machache yalisalia yanaendelea kutafutiwa ufumbuzi," alisisitiza Bi. Christina Bunini. Aidha Bunini aliongeza kwa kusema kuwa Idara pia imeendelea kuhakikisha haki na stahili za watumishi zinapatikana kwa kuwapandisha madaraja watumishi wanaostahili baadaya kupata vibali kutoka Wizara ya Utumishi na katika kipindi hicho jumla ya watumishi wapatao 2,230 walipandishwa vyeo na waliosalia wameendelea kuwekwa katika bajeti ili wakati ukifika wapandishwe vyeo".

# IDARA YA MIFUGO NA UVUVI

Idara ya Mifugo na Uvuvi ni moja ya Idara za Halmashari ya Manispaa ya Tabora inayoshughulikia maswala yote yanayohusu Mifugo na Uvuvi katika Halmashauri. Idara inafanya shughuli zake kwa kuzingatia sheria na miongozo mbalimbali. Kwa mujibu wa sheria ufugaji katika Manispaa unapaswa kuwa ufugaji shadidi **(Zero grazing)** ili kuzuia uharibifu unaosababishwa na mifugo hasa katika mazingira na Miundo mbinu mingine.

Katika kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano Idara imefanya kazi kubwa ya kuhakikisha wananchi wanafanya ufugaji wa kisasa na wenye tija zaidi kwao wao wenyewe, kwa Manispaa yetu ya Tabora na kwa Taifa letu kwa ujumla. Manispaa ya Tabora kupitia Idara ya Mifugo imeweza kukarabati Machinjio ya Halmashauri ili kulinda afya ya walaji wa nyama na kutoa huduma bora kwa Wafanyabiashara pia.

Halmashauri pia ilifanikiwa kutoa Elimu ya kuogesha mifugo kwa Kata zote hasa kwa Kata zile 4 zenye majosho na kwa Kata nyingine walipatewa Elimu namna ya kuogesha kwa kutumia mabombam jambo ambalo linafanyika mpaka kwenye vijiji vyote.



**Ujenzi wa josho ukiendelea Kata ya Kakola**

Katika kuhakikisha kila kijiji kinatenga eneo maalumu kwa ajili ya wakulima na wafugaji Elimu imetolewa na inaendelea kutolewa katika Kata 13 za nje ya Mji ambapo ni Malolo, Itetemia, Ntalikwa, Itonjanda, Ifucha, Uyui, Ndevelwa, Ikomwa, Misha, Kabila, Kalunde, Kakola na Tumbi.



Aidha Elimu imetolewa na inaendelea kutolewa kwa Wavuvi ili kuanzisha Ushirika wao katika bwawa la Igombena Kazima, na imetolewa pia kwenye baadhi ya Ktaa kama vile Kabila, Misha, Ikomwa na Ifucha.

Manispaa ya Tabora kupitia kwa wataalamu wake imeweza kuchanja ng’ombe dhidi ya Homa ya mapafu **(CBPP)** katika kata **29** za Halmashauri ili kulinda afya za wanyama dhidi ya ugonjwa huo. Jumla ya ng’ombe **39,050** walichanjwa dhidi ya homa ya mapafu kwa kipindi cha miaka mitano yaani kuanzia 2016-2019.



Aidha Idara inaendelea na shughuli ya kutoa ushauri kwa Wananchi wa Halmasahuri ya Manispaa ya Tabora kuhusu ufugaji bora na wenye tija ili kujiongezea kipato na kujiinua kiuchumi kwa kutumia Maafisa mifugo waliopo katika Kata na kujenga miundombinu bora kwa ajili ya Mifugo.

# IDARA YA KILIMO.

Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika pamoja na mambo mengine lakini Idara inatekeleza majukumu yake kwa kutoa ushauri wa kitaalamu katika **Vijiji 41** vya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na kwa Kata **zote 29** ambapo eneo linalofaa kwa kilimo ni **hekta 81,900** lakini **hekta32,134** zinalimwa mpaka sasa.

Kwa kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano Idara imekuwa ikitekeleza majukumu mbalimbali ya kutoa ushauri kwa wakulima kuhusu mbinu bora za kilimo ili kuongeza tija ya uzalishaji mazao.

Vilevile Halmashauri imeanzisha mashamba darasa ya kilimo cha mazao mbalimbali yapatayo **44**na wakulima **1,100** wamepata mafunzo na kuwaongezea ujuzi kwa lengo la kuwaltea tija katika shughurizao za kila siku.

Kwa upande waUmwagiliaji, Idara imeweza kusimamia ukamilishaji wa Mradi wa Umwagiliaji wa Inala uliopo kijiji cha Inala ambapo **Ekari 509** zimekamilika na kugawiwa kwa wakulima. Kilimo cha mpunga kimeishaanza katika Skimu hiyo ya Inala ikiwanufaisha wakulima hao **509** waliopo kijijini hapo Inala na maeneo jirani ikiwa ni pamoja na kilimo cha mazao ya bustani.

Vilevile tumeendelea kuimarisha kilimo cha Umwagiliaji kwa kufanya upembuzi yakinifu wa Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Iyombo ambayo tunatarajia kuanza ujenzi hivi karibuni, aidha skimu hii itakuwa ana hekta zipatazo **200** ambazo zitawanufaisha wakulima **500,** Skimu ya Magoweko kuna ekari **122** zinazolimwa mpunga na mazao ya bustani pia", alisisitiza Kaimu Mkuu wa Idara ndg Mwinuka.






**Shamba darasa pamoja na bwawa lililopo Kijiji cha Inala Manispaa ya Tabora**

Aidha Idara imeendelea kusimamia Ushirika ambapo katika kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano Halmashauri imeanzisha Chama cha Ushirika cha Pamba – Igosha **(AMCOS)** pamoja na kuendelea kuvisimamia vyama vya Ushirika vya Mazao **(AMCOS)** vipatavyo **vitano (5)** vya Tumbaku **(SACCOS)** zipatazo **(10)** pamoja na Vyama vya Ushirika wa Huduma vitavyo **viwili (2).**

# KITENGO CHA MAENDELEO YA UFUGAJI WA NYUKI 2016 – 2020.

Mafanikio haya yamepatikana kutokana na utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizopangwa katika kipindi hiki. Shughuli kuu zilizotekelezwa ni pamoja na utoaji wa mafunzo mbalimbali, uhamasishaji na uratibu kwa wadau wa sekta ya ufugaji wa Nyuki wakijumuisha wafugaji wa nyuki, wachakataji na wafanyabiashara wa mazao ya nyuki pamoja na taasisi za umma na binafsi. Aidha, utekelezaji huu uliendа sambamba na utekelezaji wa ***ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya 2015 ibara ya 33 'Kuendelea kutekeleza programu ya ufug aji nyuki ya mwaka 2007–2016 ili kuwajengea uwezo wadau wake kuzifahamu mbinu bora za uzalishaji wa mazao ya nyuki na pia masoko ya asali na nta ya ndani na nje ya nchi'.***

**Mafanikio yaliyopatikana yanayoonekena (tangible outcomes/outputs) ni:-**

1. Uanzishwaji wa kiwanda cha kuchakata mazao ya nyuki (Nta na Asali) chenye uwezo wa kuchakata zaidi ya tani moja kwa siku. Kiwanda hiki kinaendelea kuboresha ubora na usalama wa mazao ya nyuki ili kuwa shindani sokoni na hivo kuyaongezea thamani ambapo wachakataji na wafanyabiashara wa mazao ya nyuki watawezeshwa kujiongezea kipata chao. Aidha, mafunzo ya vitendo yatakuwa na tija. Kiwanda hiki kinamilikiwa na Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji nyuki kilichopo katika Hamashauri ya Manispaa ya Tabora.
2. Uanzishwaji wa kiwanda cha kuchakata Nta pekee kinachomilikiwa na sekta binafsi (Grand Botanical). Kiwanda hiki kina uwezo wa kuchakata tani 100 za nta kwa mwaka, lengo ni kuchakata nta kwa ajili ya kuisafirisha nje ya nchi (for export). Usafirishaji wa bidhaa hii nje ya nchi unainufaisha nchi kwa kujiongezea fedha za kigeni na wafugaji kupata soko la uhakika la Nta. Kwa wastani kiwanda kimekuwa kikichakata tani 54 za nta kwa mwaka, bidhaa zimethibitishwa na Tbs. Kiwanda hiki kipo Mtaa wa Kiloleni, Manispaa ya Tabora.
3. Uanzishaji wa kiwanda kidogo cha kuchakata Asali kinachoitwa Honey house processing centre kilichopo Mtaa wa Ipuli, Manispaa ya Tabora. Bidhaa inayotoka katika Kiwanda hiki imethibitishwa na Tbs na hivo kuwa na ubora unaotakiwa sokoni. Kiwanda kina uwezo wa kuchakata kiasi cha tani 3 kwa mwaka.
4. Upatikanaji wa mapato ya Halmashauri kutoka Tsh.0 mwaka 2015 hadi kufikia takribani Tsh. 18,000,000/- mwaka 2020.
5. Uzalishaji wa mazao ya Nyuki umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka kutegemeana na uwepo wa hali ya hewa inayostahili. Kwa wastani uzalishaji umeongezeka kutoka Tani 10 za asali na 0.5 za nta mwaka 2015 hadi kufikia Tani

109.9 za asali (sawa na Tsh. 384,650,000/- kwa wafugaji na Tsh.879,200,000 kwa wachakataji na wafanyabiashara) na 6.4 za nta (Sawa na Tsh.64,000,000/-) mwaka 2019/2020.

6. Biashara ya mazao ya nyuki imeendelea kukuwa na kuwanufaisha wafugaji wa Nyuki na wafanyabiashara wa mazao haya. Mathalani, mwaka 2015 thamani ya mazao yaliyonunuliwa na kuuzwa ilikuwa takribani Tsh. 13,000,000/-, mwaka 2018/2019 ilifikia Tsh. 96,000,000/- za asali na Tsh.70,100,000/- za nta (Sawa na ukuaji wa 93% kwa kipindi cha 2015/16 hadi 18/19 na 23.2% kwa mwaka)
7. Halmashauri imewezesha Vikundi vitano vya wafugaji wa nyuki kunufaika kwa kupata ruzuku ya Tsh. 104,000,000 kutoka Mfuko wa Misitu Tanzania. Fedha hii imetumika kununulia mizinga 420, mtambo 1 wa kuchakatia asali, kujengea mabanda 7 ya kufugia nyuki na kutolea mafunzo ya ufugaji bora wa Nyuki. Vikundi hivi ni Ecobeg-20,000,000/-, Akina mama tuinuane – 5,000,000/- (Ifucha); Ibeco-20,000,000/- (Inala), Akina mama Juhudi-20,000,000/- (Kalunde) na Miombo Beekeeping initiatives – 39,000,000/- (Masimba).
8. Uanzishwaji wa umoja wa wafugaji nyuki na wachakataji wa mazao ya nyuki (TABNET), ambao haukuwepo hapo kabla. Lengo la umoja huu ni kuwaunganisha wadau wa sekta ya ufugaji nyuki ili kuboresha ufanisi wa shughuli zao
9. Uanzishaji wa uvunaji wa sumu ya nyuki (bee venom) kimkataba kwa ajili ya kuiuzia kampuni ya ACLA kutoa Dar es salaam ambayo itaisafirisha kwenda nchi za nje. Wafugaji wa Nyuki watanufaika kwa kujiongezea kipato kwani gram 1 itauzwa kati ya Tsh. 15,000/- hadi 50,000/-. Uvunaji huu ni wa kwanza kufanyika hapa nchini hivo itakuwa model.
10. Uongezaji thamani mazao ya nyuki (value addition) umefanyika kwa wafugaji kutengeneza mafuta ya kupaka na mishumaa kutokana na mazao ya nyuki. Hali hii imeboresha upatikanaji wa kipato kwa kuwa kilo 1 ya nta huuzwa Tsh.11,000/- ambapo inaweza kutangeneza chupa 33 za mafuta ya kupaka, sawa na Tsh. 66,000.
11. Jumla ya wafugaji nyuki ni 580 (Ke-161); Mizinga ni 3,021 ya sanduku na 3,633 ya asili; Vikundi vya wafugaji nyuki 31; Vikundi vya uchakataji 18; Vyama vya umoja wa wafugaji nyuki na wachakataji 1; na Viwanda vya kuchakata mazao ya nyuki 3. Kwa ujumla ongezeko ni zaidi ya 50% ukilinganisha na mwaka 2015, (alisema Seif Salum Mkuu wa Kitengo Maendeleo ya Ufugaji wa Nyuki).





**Picha ikionesha duka la asali**

**Picha ikionesha nta ya Tabora Manispaa**





**Picha ikionesha kiwanda cha kuchakata mazao ya Nyuki-BTI**

**Picha ikionesha Manzuki**

# SEKTA YA BIASHARA NA VIWANDA

Sekta ya Biashara na Viwanda ndiyo Sekta kubwa ambayo inachangia Uchumi wa wananchi na Serikali kwa zaidi ya **asilimia 75.** Sekta ya Biashara na Viwanda ndiyo inapelekea Halmashauri ya Manispaa na Serikali kukusanya Mapato na kuweza kuendelesha shughuri za Serikali kwa ujumla.

Kwa miaka Mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano Sekta ya Biashara na Viwanda imepata mafanikio kadhaa ikiwamo;

- Kuanzisha Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato wa **LOCAL GOVERNMENT REVENUE COLLECTION INFORMATION SYSTEM** ambao umefanikisha kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kutoka **Tzs3,455,460,233,67** sawa na **asilimia368...09** ikiwa ni kutokana na kodi na tozo mbalimbali za Manispaa ya Tabora.

- Kurahisisha biashara zisizo rasmi zipatazo **8.325** kwa kuwapatia vitambulisho vya Ujasiliamali kwa fanyabiashara wadogo wadogo.

- Kupanga maeneo rasmi ya kufanyia biashara mbalimbali Kurasimisha barabara ya Salmini kwa siku mbili za mwisho wa wiki ili kusaidia wafanyabiashara wadogo wadogo kufanya biashara zao. Pia kupanga maeneo rasmi na kuboresha mazingira ya biashara katika maeneo hayo, aidha kuanzishwa kwa soko jipya la kushushia mazao ya nafaka na matunda ya jumla Tambukareli na Soko la Mbao eneo la Transifoma Kata ya Ipuli.

- Kuboresha Mazingira ya Biashara kwa kutoa fedha ili kujenga kituo kimoja cha biashara kitakachoweza kusaidia kupunguza gharama za kufuatilia nyaraka za Serikali kwa Wafanyabiashara na kupunguza muda wa kufuatilia na kukamilisha nyaraka hizo.

# IDARA YA MAZINGIRA

Idara ya Mazingira ni kati ya Idara muhimu katika Halmashauri ambayo husimamia na kuratibu shughuli za Usafi wa Mazingira ya Halmashauri. Halmashauri itaendelea kusimamia Sheria, taratibu na kanuni za mazingira na ushirikishwaji wa Jamii katika kutunza na kuhifadhi mazingira katika maeneo yao.

Katika kuhakikisha usafi wa mazingira unakuwa endelevu Halmashauri inaendelea kuhamasisha wananchi, taasisi za umma na binafsi kufanya usafi wa mazingira maeneo yanayowazunguka ili kudhibiti magonjwa nyemelezi yatokanayo na uchafu wa mazingira haswa utupaji wa taka ovyo mitaani na utiririshaji wa maji taka maeneo mengine ambapo usafi umepewa kipaumbele vilevile ufyekaji wa nyasi ndefu wakati wa masika na Upandaji Miti. kwa kipindi cha mwaka 2016 – 2020 Idara imefanikiwa kufanya yafuatayo:

**KUFANYA KAMPENI YA USAFI WA MAZINGIRA KATIKA KATA ZOTE 29 ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA IFIKAPO JUNI 30, 2020.**

Halmashauri inasimamia swala la kufanya kampeni ya usafi wa Mazingira kupitia wataalam wake kwenye maeneo yao ya Kazi ambapo inafanyika kila siku na Maafisa Mazingira, Maafisa Afya, watendaji wa Kata, watendaji wa Mitaa na vijiji kwenye kata zote 29, mitaa 134 na vijiji 41 vya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

Tangu mwaka 2016 ilipo agizwa na Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt John Pombe Magufuli kuwa kila jumamosi ya mwisho wa mwezi itakuwa siku ya Usafi wa Mazingira Nchi nzima, Halmashauri imeendelea kutekeleza Kusimamia, kuhimiza na kukagua usafi wa kila jumamosi ya mwisho wa mwezi agizo hili ambapo lilikuja kutungiwa sheria na kutangazwa kwenye gazeti la serikali GN. 139 ya tarehe 22/4/2020 CAP (191).

Kazi hii inafanyika kila jumamosi ya mwisho wa mwezi ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi Manispaa Kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya, Wakuu wa Idara na watumishi wote na wananchi kwa ujumla, ambapo kwa sasa watu wengi wameelewa na wanazingatia utekelezaji wa sheria hii.

**KUINUA KIWANGO CHA UKUSANYAJI, NA UTUPAJI TAKA NGUMU KATIKA KATA 17 ZA MANISPAA YA TABORA TOKA TANI 33,924 HADI 49,476,6 KWA MWAKA.**

Halmashauri imefanikiwa Kuinua kiwango cha ukusanyaji, usafirishaji na utupaji taka ngumu kutoka tani 7,560 kwa mwaka 2015/2016 hadi tani 40,720 kwa mwaka 2019/2020 sawa na asilimia 82.3ya lengo la kukusanya tani 49,476.6. Ongezeko hili la uwezo wa kuzoa taka ngumu kutoka kwenye vizimba (collection points) na kwenye Kaya limetokana na Halmashauri kuwa na vifaa/mitambo kwa ajili ya taka ngumu. Mitambo hiyo ni pamoja naMotor Greda 1, Skip Truck 2, Skip Bins 40, Excavator 1, Dump Trucks 2. Vifaa hivyo vimetokana na Mradi wa ULGSP na vimekuwa na msaada mkubwa katika kuongeza uwezo wa Halmashauri kwenye uzoaji wa taka ngumu.

**KUBINAFSISHA SUALA LA UKUSANYAJI NA UZOAJI TAKA KWENYE KAYA KATIKA MJI WA TABORA.**

Halmashauri katika kipindi cha mwaka 2015 – 2016 kulikuwa hakuna vikundi kutokana na miundombinu na vituo rasmi vya kutupia taka (collection point) ambapo kulikuwa na vituo 13 tu lakini hadi sasa mwaka 2020 kuna vituo 12

vilivyoongezeka na kufanya kuwa 25 na skip bins 40 hata hivyo Halmashauri katika mwaka wa fedha 2020/2021 imeamu kutangaza Zabuni ya usafi wa mazingira kwa ajili ya kupata makampuni makubwa ya kukusanya taka toka kwenye kaya kupata vikundi vya kijamii, Taasisi, watu binafsi lengo nikuweka mji safi na kukuza ajira za vijana wenye ujuzi na wasio na ujuzi.

Halmashauri ipo kwenye hatua za mwisho kwa ajili ya Kubinafsisha shughuli za usafi na mazingira kwa makampuni, Vikundi, Taasisi na watu binafsi lengo kuongeza ufanisi kwenye ukusanyaji mapato na kuweka mji safi kwa kuweza kufikia kaya kwenye uzoaji taka kama ilivyo kwenye jiji la Dodoma, Arusha, Dar es Salaam, Mwanza na Manispaa ya Moshi. Halmashauri itabaki kuzoa taka kwenye vituo vya taka ambako kutakuwa na vikundi vya kijamii Suala la ubinafsishaji shughuli za usafi wa mazingira

Endapo litafanikiwa kwa asilimia 90-100 litawezesha Halmashsuri kukusanya mapato mengi ya tozo za taka Ngumu pia itafanikisha Manspaa ya Tabora kuwa safi na yenye mandhari Mazuri.

**KUSIMAMIA MIONGOZO, SERA, MPANGO NA PROGRAMU YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA SHERIA ZA USIMAMIZI WA MAZINGIRA.**

Halmashauri imesimamia ugawaji wa sera, miongozo, Sheria na Kanuni mbalimbali kwenda kwenye ofisi za kata, vijiji/mitaa na jamii kwa ujumla.Kusimamia zoezi la zuio la plastiki, kuadhimisha siku ya mazingira duniani kila mwaka na kusimamia ugawaji wa majiko banifu 500 kwa majasiriamali wanaotoa huduma ya baba na Mama Lishe na majiko 8 kwenye shule za bweni (Tabora boys na Tabora Girls) kwa ajili ya kutekeleza sera ya kuhifadhi mazingira kutoka kwa mdau wa mazingira KIKUNDI CHA KUJA NA KUSHOKA.

Aidha Halmashauri itaendelea kuhakikisha inasambaza miongozo, sheria na Kanuni kadri inavyopokelewa lengo ni kuhakikisha usimamizi wa usafi na uhifadhi mazingira unafuatwa kwa mujibu wa sheria, sera na Katiba ya jamuhuri ya muungano wa Tanzania.

**KUSIMAMIA UPANDAJI MITI, UTUNZAJI WA MITI ILIYOPANDWA NA YA ASILI KWENYE KATA 29 NA BARABARA ZOTE ZA MANISPAA.**

Katika kipindi cha miaka 5, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ililenga kupanda miti 7,500,000 ambapo imefanikiwa kupanda miti 5,858,453 sawa na asilimia 78 ya lengo. Miti hiyo imepandwa kwenye maeneo yote ya Manispaa ya Tabora. Miti hiyo imepandwa kwa kushirikiana na makampuni ya Tumbaku, Vyama vya Ushirika, Vyama vya Siasa, Shule za Msingi na Sekondari, Watu Binafsi, Wakulima wa Korosho, TFS, TUWASA, TANROAD, TEMESA na kwenye kata 29, Mitaa 134 na Vijiji 41.

Halmashauri imeendelea kusimamia utunzaji wa miti iliyopandwa na asili kwa kudhibiti uchomaji moto ovyo, ukataji miti ovyo, uzururaji wa mifugo mjini, kupalilia visahani kwenye miti ilipandwa na kuendelea kutoa elimu umuhimu wa utunzaji mazingira kwa vizazi vya sasa na vijavyo.





**Pich ikionesha miche iliyo katika moja kati ya vitalu na baadhi ya miti iliyokwisha pandwa katika baadhi mitaa.**

## KUSIMAMIA UNYONYAJI WA MAJI TAKA, USAFIRISHAJI WA MADIMBWI, MITARO YA MAJI NA UPENDEZEZAJI MJI IFIKAPO MWAKA 2020.

Halmashauri imefanikiwa kuinua huduma ya usafirishaji wa maji taka toka kwenye vyoo vya umma na vya watu binafsi kwa kutumia gari ya Halmashauri ambapo jumla ya lita 6,435,000 zimenyonywa na kusafirishwa kwenda eneo la kuhifadhi maji taka kulinganisha na kiasi cha lita 1,157,000zilizonyonywa msimu wa 2015/2016. Barabara zote za Manispaa na maeneo ya wazi yanasafishwa na kipindi cha Masika yanafyekwa kwa ajili ya kuweka mji safi pia mizunguko yote ya Manispaa kwa sasa inaboreshwa kwa kupandwa majani na baadae maua mbalimbali ili kuongeza upendezeshaji wa mji (Beutification). Mafanikio haya yametokana na ukarabati wa gari la maji taka kwa kulinunulia matairi mapya pia kudhibiti unyonyaji wa majitaka kwenye vyoo vya umma kwa kuhakikisha vinatumia gari la Halmashauri kila vinapohitaji huduma hii imepunguza gharama na kusaidia kupatikana kwa takwimu sahihi ya ujazo wa maji taka yaliyonyonywa. Halmashauri inaitaji gari jingine jipya ili kuongeza ufanisi zaidi kutokana na mji kuendelea kukua kwa kasi. Halmashauri ipo hatua za mwisho kutangaza zabuni ya kuingia ubia kwa ajili ya kuziendesha na kuzitunza hii itawezesha Halmashauri kupata mapato na mandhari mazuri ya mji.

## KUONGEZA MAPATO YA HALMASHAURI KWA KUKUSANYA USHURU WA MADINI YA UJENZI, TAKA NGUMU, MAJI NA FAINI ZINAZOTOKANA NA UHARIBIFU WA MAZINGIRA IFIKAPO JUNE 2020.

Halmashauri kupitia Idara ya usafi na mazingira katika Mwaka wa fedha 2015/2016 ilikuwa na bajeti ya kukusanya kiasi kisichozidi Tshs milioni 50 na ilikuwa na vyanzo viwili 2 (ushuru wa gari la maji taka na tozo ya taka ngumu) mwaka 2017-2018 Idara ilibuni na kuongeza vyanzo viwili (2) vipya (Ada ya mazingira na madini ya ujenzi) na kuboresha ushuru wa maji taka ambapo Halmashauri ilivilipitisha vyanzo hivyo hadi kufikia mwaka 2019/2020 Idara imefikia bajeti ya tshs 344,190,000.00. makusanyo kama ifuatavyo:

| CHANZO | MAKISIO YA BAJETI 2019 -2020 | MAKUSANYO HALISI HADI JUNI 2020 | % |
|---|---|---|---|
| **Ushuru wa taka ngumu** | 84,016,000.00 | 84,291,911,31 | 100.33 |
| **Faini** | 18,000,000.00 | 12,897,200.00 | 71.65 |
| **Ushuru wa madini ya ujenzi** | 8,400,000.00 | 7,351,900.81 | 87.52 |
| **Maji taka** | 210,384,000.00 | 149,286,300.00 | 70.96 |
| **Ada ya mazingira** | 23,390,000.00 | 19,562,172.00 | 83.63 |
| | **344,190.000.00** | **273,389,484.14** | **79.42** |

# MIRADI/PICHA



DC Tabora Mjini Mh. Komanya Kitwala akikabidhi Bima za Afya kwa watoto wenye mahitaji maalum S/M Furaha



Baadhi Ya Wawakilishi Wa Benki ya Dunia wakiwa kwenye kikao na watumishi wa Manispaa Ya Tabora




Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora Ndugu Bosco Ndunguru (mbele kulia) akiwa na wageni wa Benki ya duniai.



DC Komanya Kitwala wa Tabora Mjini aliye simama akieleza jambo katika ufunguzi wa kituo cha pamoja (One Stop Center)



Aliyekuwa Diwani Kata ya Chemchem Mh. Rehema Kabata (wa pili kushoto walio kaa) akiwa na Mkuu wa Usalama Barabarani Mkoa wa Tabora, ASP Gabriel Chiguma akiwa na maafisa wengine wakati wa utoaji wa elimu ya Usalama barabarani kwa mawakala wa mabasi.



Moja kati ya mtandao wa barabara za lami KM 23.5 zilizojengwa katika Manispaa ya Tabora